JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA AFYA

*Idara ya Kinga · Sehemu ya Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa*

**WIKI 33 · 2026**

# JARIDA LA JAMII

**10 — 16 Agosti 2026**




**Ramani ya Tanzania, ikionesha mtawanyiko wa Magonjwa ya mlipuko na matukio yenye athari kiafya yaliyojitokeza katika mikoa mbalimbali, wiki ya kiepidemiolojia ya 33, 2026.**

| 524 | 2 | 141 | 11 | 1 |
|---|---|---|---|---|
| Kung'atwa na Mbwa/Paka | Visa vya Surua | Kung'atwa na Nyoka | Homa ya Dengue | Kisa cha Influenza |

Piga simu 199 (bure) kutoa taarifa ya tukio lolote la kiafya katika jamii

# Yaliyomo


1. **Magonjwa ya Mfumo wa Njia ya Hewa** — Uk. 3
2. **Magonjwa Yanayozuilika kwa Chanjo** — Uk. 4
3. **Kung'atwa na Mnyama Jamii ya Mbwa/Paka** — Uk. 5
4. **Kung'atwa na Nyoka** — Uk. 6
5. **Homa ya Dengue** — Uk. 7


## Kwa Nini Jarida Hili?

Kila wiki, Wizara ya Afya inafuatilia magonjwa yanayoweza kuathiri jamii yetu. Jarida hili linakupa taarifa fupi na sahihi kuhusu magonjwa haya, hatua ambazo Serikali inachukua, na — muhimu zaidi — unachoweza kufanya wewe kujikinga na kulinda familia yako.

### Magonjwa ya Mlipuko na Matukio yenye Athari za Kiafya Duniani

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo:** Mlipuko wa Ebola aina ya Bundibugyo umendelea kuwa tishio kubwa, visa vikifikia 4,381 na vifo 2,011; Shirika la Afya Dunia imebaini kuwa mlipuko huenda ulianza mapema Februari 2026 kutokana na baadhi ya visa vya awali kutotambuliwa.

**Nigeria:** Imeripoti visa 1,000 vya homa ya Lassa na vifo 237.

**Hispania:** Homa ya Kuvuja Damu ya Crimean-Congo imeendelea kuripotiwa.

**Urusi:** Visa vya homa vya kuvuja damu vimeongezeka .

**Bangladesh:** Dengue umeendelea kuongezeka, ikiwa na zaidi ya wagonjwa 21,000 waliolazwa na vifo 63, Pia visa vya Surua vimeripotiwa zaidi ya 17,000 vilivyothibitishwa na vifo 880.

**Ufaransa:** Imeripoti maambukizi ya Chikungunya na Dengue.

**Marekani:** Tahadhari imetolewa kuhusu ongezeko kubwa la Surua.

# Magonjwa ya Mfumo wa Njia ya Hewa

Kwa wiki ya 33, jumla ya sampuli 81 za wagonjwa wa mfumo wa njia ya hewa zilipimwa vipimo vya Influenza na UVIKO-19. Majibu ya vipimo vya magonjwa ya njia ya hewa yanaonesha uwepo wa kiwango kidogo cha maambukizi ukilinganisha na miezi mingine (low season), mwenendo ambao umeonekana hata kwa miaka iliyopita.

**1/81**
Sampuli chanya za Influenza (1.2%)

Hakuna ongezeko ukilinganisha na wiki iliyopita

**0**
Vifo vilivyoripotiwa

## Mikoa Zilizoripoti

Mbeya

## Dalili za Kuzingatia

- Kuumwa Kichwa
- Homa
- Uchovu
- Kikohozi
- Mafua

## Hatua zilizochukuliwa

- ✔ Kuimarisha ufuatiliaji katika vituo vya sentinel kwa kuchukua sampuli za wagonjwa wanaofika.

### Wito kwa Jamii

- → Osha mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji safi, au tumia vitakasa mikono.
- → Funika mdomo na pua unapokohoa/kupiga chafya — tumia tishu au kiwiko cha mkono.
- → Fika kituo cha afya mapema endapo una homa, kikohozi, mafua makali au kupumua kwa shida.

# Magonjwa Yanayozuilika kwa Chanjo

Sampuli 2 kati ya 62 (3.2%) zilionesha uwepo wa vimelea vya Surua wiki hii. Idadi hii haijafikia kiwango cha mlipuko, lakini uangalifu unaendelea.

| 2/62 | ➡ | 0 |
|---|---|---|
| Sampuli chanya za Surua (3.2%) wiki hii | Haijafikia kiwango cha mlipuko | Vifo vilivyoripotiwa |

## Halmashauri Zilizoripoti

- Wilaya ya Arusha — **Kisa 1**
- Wilaya ya Maswa— **Kisa 1**

## Dalili za Kuzingatia

- **Homa Kali**
- **Macho Mekundu**
- **Mafua/Kikohozi**
- **Vipele Mwilini**

## Hatua zilizochukulia

- ✔ Utoaji wa chanjo kwa watoto.
- ✔ Elimu kwa jamii kuhusu magonjwa na umuhimu wa chanjo.
- ✔ Matibabu sahihi kwa wagonjwa wote wenye dalili za ugonjwa.
- ✔ Utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto wanaopatiwa chanjo.

### Wito kwa Jamii

→ Peleka mtoto wako kwenye chanjo kwa kufuata ratiba yake.

→ Toa taarifa haraka pale mtoto anapoonesha dalili za ugonjwa.

→ Shiriki kikamilifu kwenye kampeni za chanjo zinazofanyika jirani yako.

# Kung'atwa na Mnyama Jamii ya Mbwa/Paka

Matukio ya watu 524 ya kung'atwa na mnyama jamii ya mbwa na paka wanaoweza kusababisha ugonjwa wa kichaa cha mbwa, bila kifo yametolewa taarifa wiki hii ya 33. Idadi hii imeongezeka kwa asilimia 14.7 ikilinganishwa na matukio ya watu 457 kung'atwa yaliyotolewa taarifa wiki ya 32. Bado ni idadi kubwa inayohitaji tahadhari.

| 524 | ↑ | 0 |
|---|---|---|
| Watu waliong'atwa na mbwa/paka wiki hii | Ongezeko 14.7% ukilinganisha na wiki iliyopita | Vifo vilivyoripotiwa |

## Mikoa Yenye Matukio Mengi

Dodoma — **49** | Mara — **49** | Mwanza — **47** | Arusha — **34** | Singida — **34**

## Uking'atwa, Fanya Hivi

**Uking'atwa na Mnyama** → **Osha Jeraha kwa Sabuni na Maji** → **Nenda Kituo cha Afya Haraka**

## Hatua zilizochukulia

- ✔ Kuimarisha upatikanaji wa chanjo ya Kichaa cha Mbwa kwa binadamu.
- ✔ Wahudumu wa afya kuendelea kutoa elimu kuhusu kujikinga na hatua za kuchukua baada ya kung'atwa.
- ✔ Wananchi wanaofuga wanyama jamii ya mbwa na paka wahakikishe wanachanja wanyama hao kila mwaka.

### Wito kwa Jamii

→ Osha jeraha kwa sabuni na maji mengi kabla ya kwenda hospitali; usifunge jeraha.

→ Fika kituo cha afya mara moja kwa matibabu na chanjo pale inapohitajika.

→ Wamiliki wa mbwa/paka — wachanje wanyama wenu dhidi ya Kichaa cha Mbwa kila mwaka.

# Kung'atwa na Nyoka

Jumla ya watu 141 wametolewa taarifa ya kung’atwa na nyoka bila kifo katika wiki ya 33. Idadi hii imepungua kwa asilimia 19.9 ikilinganishwa na matukio 176 ya wiki ya 32.

| | | |
|---|---|---|
| **141** | ↓ | **0** |
| Watu waliong'atwa na nyoka wiki hii | Imepungua 19.9% ukilinganisha na wiki iliyopita | Vifo vilivyoripotiwa |

## Mikoa Yenye Matukio Mengi

Dodoma — **19** · Kagera — **18** · Tanga — **17** · Lindi — **14** · Morogoro — **13**

## Jikinge Nyumbani

- **Tumia Mwanga Usiku**
- **Safisha Mazingira**
- **Vaa Mabuti/Glavu**
- **Lala Katika Kitanda Vilivyo Juu**

## Hatua zilizochukulia

- ✔ Sehemu ya Epidemiolojia inaendelea kuwasilisha taarifa za matukio kwa Mkurugenzi wa Tiba na wadau husika.
- ✔ Taarifa hizi zinatumika kuhakikisha upatikanaji wa dawa kingi dhidi ya sumu ya nyoka (anti-venoms) katika mikoa yenye matukio mengi.

### Wito kwa Jamii

→ Nenda kituo cha afya mara moja — usipoteze muda.

→ Usitumie dawa za kienyeji wala kubana mshipa wa damu kwenye jeraha.

→ Kumbuka muonekano wa nyoka (rangi/umbo) bila kuhatarisha usalama wako — itasaidia matibabu.

# Homa ya Dengue

Kwa wiki ya 33, Wizara imepokea taarifa ya wagonjwa  6 kutoka Mkoa wa Dar es Salaam; Kinondoni (5) na Ilala (2), Kigamboni (2), Ubungo (2), idadi hii imeongezeka ukilinganisha na wiki iliyopita ambapo kulikuwa na wagonjwa 2.

| | | |
|---|---|---|
| **6** | ⬆ | **0** |
| Wagonjwa wiki hii | Imeongezeka ukilinganisha na wiki iliyopita | Vifo vilivyoripotiwa |

## Mikoa Zilizoripoti

Dar es Salaam

## Dalili za Kuzingatia

- **Homa ya Ghafla**
- **Maumivu ya Viungo**
- **Uchovu Mkali**
- **Maumivu ya Kichwa**

## Hatua zilizochukulia

- ✔ Kuongeza upatikanaji wa vipimo katika vituo vya afya.
- ✔ Kushirikiana na Halmashauri na wadau kuhakikisha usafi wa mazingira.

### Wito kwa Jamii

→ Mwaga maji yaliyotuama kwenye madumu, mapipa na vyombo vingine.

→ Weka mazingira safi — ondoa taka zinazoweza kuzalisha mbu.

→ Fika kituo cha afya haraka ukipata homa ya ghafla, maumivu ya viungo, au uchovu usio wa kawaida.

# MTU NI AFYA

Jamii bora huzingatia kanuni muhimu za afya. Asante kwa kusoma na kushiriki taarifa hizi na jirani, familia na marafiki zako.

Wizara ya Afya
Idara ya Kinga
Sehemu ya Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa

Una tetesi au tukio la kiafya? Piga simu bure:

**199**

Huduma hii ni ya bure saa 24